



UNACHOHITAJI KUJUA KUHUSU
—— VIKWAZO VYA ——

“KULINDA MAISHA
KATIKA USAIDIZI WA
KIMATAIFA WA AFYA”
KWA MSAADA WA KIMATAIFA
UNAOFADHILIWA NA MAREKANI

—— *Mwongozo Usio Rasmi* ——

UTANGULIZI

Tarehe 23 Januari, 2017, Rais Donald Trump alitia saina “Agizo la Rais kuhusu Sera ya Jiji la Mexico.” Agizo hilo limerejesha upya utekelezaji wa Sera ya Jiji la Mexico iliyokuwa ikitumika chini ya serikali ya Rais George W. Bush (miaka ya 2001-2009) na limemwelekeza Waziri wa Mambo ya Nje kwa kushirikiana na Waziri wa Afya na Huduma za Jamii “kutekeleza mpango wa kuingiza miongozo ya sera hiyo katika idara na taasisi zote zinazochangia Mpango wa Afya wa Kimataifa unaofadhiliwa na Marekani.”

Sera ya Jiji la Mexico na vizuizi vyake vilipewa jina jingine, “Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya wa Kimataifa” (ambao wakosoaji wake huita Agizo la Rais Trump kuhusu Msaada wa Afya wa Kimataifa - agizo linalokatiza matumizi ya fedha za serikali na mashirika katika kushughulikia maswala ya utoaji mimba) na hivyo basi kuitwa *sera* katika waraka huu. *Sera hii* inazuia Msaada wa Afya wa Kimataifa unaofadhiliwa na serikali ya Marekani kutolewa kwa asasi za kigeni zisizo za kiserikali (NGOs) zinazojishughulisha na utoaji mimba katika hali ambayo mimba hiyo si tishio kwa uhai wa mwanamke, au isiyotokana na ubakaji au kujamiiana kwa maharimu; kutoa ushauri nasaha (ikiwemo ushauri au taarifa) na/au kutoa rufaa ya kutoa mimba; au kushawishi katika kuhatalisha utoaji mimba au kufanya zoezi hilo kuwa rahisi katika nchi zao, hata kama shughuli hizi zinafadhiliwa na mashirika au wadau wa kimarekani walio nje ya serikali ya Marekani. Katika serikali zilizopita chini ya chama cha Republican, vizuizi hivi vilihusu msaada unaotolewa na serikali ya Marekani kwa ajili ya uzazi wa mpango. Serikali ya sasa ya Rais Trump imeamuru vizuizi hivi viwekwe katika mpango mzima wa Msaada wa Afya wa Kimataifa unaofadhiliwa na serikali.

Asasi za kigeni zisizo za serikali (NGOs) (zinazoendeshwa na zisizoendeshwa kwa faida), ambazo hazikuundwa chini ya sheria za Marekani, zinaweza kujihusisha na baadhi ya shughuli za utoaji mimba na bado zikastahiki kupata misaada chini ya mpango wa Msaada wa Afya wa Kimataifa unaofadhiliwa na serikali ya Marekani. Kipeperushi hiki kinatoa ufafanuzi wa vizuizi vilivyowekwa chini ya *sera hii* (Agizo la Rais) ili kulinda na kuhifadhi huduma muhimu sana za kuokoa maisha za kiafya na kuzuia tafsiri pana juu ya nini *sera hii* inahimiza kifanyike au inakataza.

WIGO WA SERA

Kuanzia tarehe 15 Mei 2017, *sera hii* inahitaji asasi za kigeni zisizo za kiserikali kuafiki na kuzingatia masharti yake kama sharti la kupokea msaada chini ya Msaada wa Afya wa Kimataifa unaofadhiliwa na serikali ya Marekani kwa ajili ya kutatua changamoto za dharura za afya ya umma zifuatazo:

- VVU/UKIMWI, ukiwemo Mpango wa Msaada wa Dharura wa Rais wa Kupambana na UKIMWI (PEPFAR);
- Kifua kikuu;
- Malaria, ikiwemo Mpango wa Rais wa Kupambana na Malaria (PMI);
- Janga la homa ya mafua na hatari zingine, pamoja na ulinzi wa afya ya ulimwenguni;
- Magonjwa ya nchi za Tropiki yaliyopuuzwa pamoja na magonjwa mengine ya kuambukiza;
- Maradhi yasiyoambukiza;
- Uimarishaji wa mfumo wa afya;
- Afya ya mama na mtoto;
- Uzazi wa mpango na afya ya uzazi;
- Shughuli za usafi wa binafsi, makazi na mazingira katika jamii, pamoja na maswala ya maji; na
- Lishe.

Taasisi ambazo *sera hii* haitawahusu ni pamoja na (maelezo ya kina yametolewa katika vipengele vitakavyofuata):

- Mashirika ya Kimarekani yasiyo ya kiserikali
- Serikali za kigeni; na
- Mashirika ya kimataifa na “taasisi nyingine za kimataifa ambazo mataifa yanayojitawala hushiriki,” kama vile Mfuko wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria Duniani, na vile vile Gavi, Ushirika wa Kimataifa wa Chanjo.

Mipango au shughuli zingine ambazo *sera hii* haitumiki ni pamoja na:

- Huduma za utoaji mimba au ushauri na rufaa ya utoaji mimba katika hali hatarishi kwa maisha, na panapotokea ubakaji au kujamiiana kwa maharimu;
- Huduma baada ya utoaji mimba, ikiwa ni pamoja na “matibabu ya majeraha na maradhi yanayosababishwa na utoaji mimba kisheria au kinyume na sheria”;
- Msaada wa kibinaadamu, ikiwa ni pamoja na maswala ya uhamiaji and misaada kwa wakimbizi chini ya Wizara ya Mambo ya Nje, pamoja na Shirika la Misaada la Kimataifa la Marekani (USAID) na Wizara ya Ulinzi, maafa na shughuli za huduma za kibinaadamu;
- Chakula kwa Amani (P.L. 480), mipango, msaada wa chakula kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya dharura na kwa maendeleo;
- Utafiti wa kimsingi wa afya;
- Matumizi ya miundombinu ya usafi wa kimazingira na maji katika baadhi ya makazi, shule, vituo vya afya, na kwa matumizi ya viwanda na biashara, na vile vile shughuli za uendelezaji wa sera ya kitaifa na za kiutawala; na
- Mpango wa Shule na Hospitali za Marekani zilizoko nje ya Nchi.

Asasi zisizo za kiserikali za Marekani zinaweza kuendelea kutoa huduma za rufaa, ushauri kwa ajili ya swala la utoaji mimba, na kushawishi upatikanaji wa fedha kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali bila ya kuhatarisha ustahiki wa kupokea msaada kutoka Msaada wa Afya wa Kimataifa unaofadhiliwa na Marekani. Sharti pekee lililowekwa na sera hii kwa mashirika na asasi za Kimarekani zisizo za kiserikali *ni kuhakikisha kwamba* washirika wao na asasi za kigeni zisizo za kiserikali, zinazopata ufadhili wa Msaada wa Afya wa Kimataifa unaogharimiwa na serikali ya Marekani.

WAKATI WA UTEKELEZAJI

Asasi za kigeni zisizo za kiserikali zinazopata ufadhili kutoka msaada wa afya wa kimataifa wa Marekani, zinawajibika kuzingatia sera hii na zinapaswa kuhakikisha zinaafiki vipengele vipya *katika makubaliano yao* ili kupokea Msaada wa Afya wa Kimataifa unaotolewa na serikali ya Marekani. Hii itafanyika pale ambapo asasi za kigeni isiyo ya kiserikali itakumbwa na hitaji jipya la ufadhili mnamo au baada ya tarehe 15 Mei 2017, ama kwa kupewa msaada mpya au makubaliano ya ushirikiano au wakati wa kufanya marekebisho ya makubaliano ya ushirikiano “ili kuongeza fedha zaidi” au “au kuongeza fedha mpya.” Sera haitatumika kwa ufadhili ambao tayari umeshatolewa kwa asasi za kigeni isiyo ya kiserikali (inayopokea ufadhili moja kwa moja au kupitia shirika jingine) chini ya mikataba iliyopo sasa au makubaliano ya ushirikiano.

Asasi zisizo za kiserikali za Marekani hazilazimiki kuhakikisha kwamba washirika wao wa nje wanafuata hii hadi pale ambapo asasi hiyo ya kimarekani imeridhia vipengele vipya katika sera hiyo *katika makubaliano yao* na serikali ya Marekani. Kwa asasi za kigeni zisizo za kiserikali, hili litatokea pale ambapo asasi isiyo ya kiserikali ya Marekani itakapohitaji ufadhili wa rasilimali fedha, ama kuingia katika majadiliano kuhusu mkataba mpya au makubaliano ya ushirikiano, au pale ambapo makubaliano ya ushirikiano yanafanyiwa marekebisho “ili kuongeza rasilimali fedha” au “kupata ufadhili mpya.”

Mashirika huashiria kuwa yanakubali kuzingatia masharti ya *sera hii* kwa kukubali vipengele vinavyoambatana na msaada wanaopokea. Hakuna hati tofauti inayohitajika.

MASHIRIKA YA KIMATAIFA YANAYOHUSISHA SERIKALI MBALIMBALI AU YA UMMA KAMA VILE SHIRIKA LA AFYA ULIMWENGUNI, SHIRIKA LA IDADI YA WATU LA UMOJA WA MATAIFA (UNFPA), NA VILE VILE MASHIRIKA MENGINE YA KIMATAIFA KAMA VILE MFUKO WA DUNIA WA KUPAMBANA NA UKIMWI, KIFUA KIKUU NA MALARIA, NA PIA USHIRIKA WA CHANJO WA KIMATAIFA (GAVI), THE VACCINE ALLIANCE, HAYAHUSISHWI KATIKA UZINGATAJI WA *SERA HII*

LUGHA YA KISHERIA INAYOTUMIKA KATIKA *SERA HII*

Lugha ya kisheria inayotumiwa na idara za serikali ya Marekani na taasisi kama vile shirika la Misaada ya Kimataifa la Marekani (USAID), Wizara ya Mambo ya Nje, Taasisi za Kitaifa za Afya (NIH), Vituo vya Udhambi na Uzuiaji wa Magonjwa (CDC) na Wizara ya Ulinzi (DoD)—inayahitaji asasi na mashirika za kigeni yasiyo ya kiserikali kukubali kuwa katika kipindi ambacho watakuwa wanapokea msaada wa afya wa kimataifa unaofadhiliwa na Marekani “hawatajijhusisha na shughuli za utoaji mimba au kushiriki katika kuendeleza utoaji mimba kama mbinu ya kupanga uzazi” au “kutoa msaada wa kifedha kwa shirika lolote la kigeni lisilo la kiserikali linalofanya vitendo kama hivyo.”

Kuhusu kifungu cha “msaada wa kifedha”, *sera hii* inatoa maelezo ya kina ya utaratibu unaopaswa kufuatwa, masharti kwa mkandarasi kuhusu ufuatiliaji wa shughuli kwa asasi zinazopokea msaada wa afya wa kimataifa unaofadhiliwa na Marekani. *Sera hii* haitoi maelezo yoyote ya jinsi inavyopaswa kutumika katika hali mbali mbali, na mpaka sasa, serikali ya Marekani haijatoa mwongozo wowote rasmi kuhusu suala hili. Hata hivyo, asasi nyingi zisizo za kiserikali ambazo PAI imezungumza nazo zinaiielewa *sera hii* kumaanisha kuwa hazipaswi kutoa rasimili fedha kwa asasi nyingine yoyote kufanya shughuli zinazohusiana na utaoji mimba, kwavile kwa kufanya hivyo itakuwa imekiuka *sera hii*.

Marufuku zinazoendelea kutekelezwa za matumizi ya moja kwa moja ya fedha za msaada wa kigeni zinazotolewa na Marekani kwa shughuli nyingi zinazohusiana na utoaji mimba (Marekebisho ya Sheria ya Helms ya mwaka wa 1973 na marufuku nyingine ndani ya kanuni za kisheria) zitaendelea kutekelezwa. [Pitia orodha kwa maelezo ya ziada.]

ASASI ZISIZO ZA KISERIKALI ZINAZOLAZIMIKA KUZINGATIA *SERA HII*

Asasi za kigeni zisizo za kiserikali (za kibiashara na zisizo za kibiashara) zinazopokea Msaada wa Afya wa Kimataifa—ama kwa kupitia ofisi za serikali ya Marekani katika nchi hizo, wakala unaoshirikiana na Marekani, asasi isiyo ya kiserikali ya Marekani au shirika mwenza katika nchi ya kigeni—yanapaswa kupitia kwa karibu makubaliano ya ufadhili, makubaliano ya ushirikiano, mikataba ya ufadhili ili kuamua iwapo *sera hii* ni sharti au hitaji la kupokea msaada. Ikiwa ni hivyo, asasi za kigeni isiyo ya kiserikali italazimika kufuata masharti ya *sera hii* katika mipango yake yote, bila kujali chanzo cha ufadhili wake. Msaada unatafsiriwa kujumuisha sio rasimili tu bali pia utoaji wa msaada wa kiufundi, mafunzo maalum, bidhaa na vifaa.

Kandarasi na asasi na mashirika ya kigeni yasiyo ya kiserikali hatimaye yatapaswa kuzingatia *sera hii*. Hata hivyo, uundaji wa sharti litakalojumuishwa katika kandarasi utakuwa ni matokeo ya mchakato wa utengenezaji wa kanuni utakaohusisha mashirika mbalimbali na ambao bado haujatanzwa, na muda utakaochukua haujulikani. Hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2017, *sera hii* haijatumika kwa kandarasi mbali mbali.

ASASI ZISIZO ZA KISERIKALI ZISIZOLAZIMIKA KUZINGATIA *SERA HII*

Asasi za kigeni isiyo ya kiserikali inayopokea rasimili fedha kutoka Msaada wa Afya wa Kimataifa unaogharimiwa na Marekani, kwa ajili ya vifaa na huduma (kwa mfano kompyuta, usimamizi au bidhaa za ofisini) kwa mpokeaji mkuu au mpokeaji mdogo wa Msaada huo halazimiki kuzingatia kipengele katika sera hiyo. Mashirika mengine ambayo hayatahusika pia ni yale ambayo yana mtu mmoja anayeshiriki katika “mpango wa jumla wa mafunzo” wa shirika linalopokea msaada wa afya wa kimataifa unaogharimiwa na serikali ya Marekani (hivyo ni kusema, shughuli ya mafunzo ya jumla inayohusisha washiriki binafsi kutoka kwa shirika).

HAZHUSIKI SERIKALI ZA KIGENI NA MASHIRIKA YA KIMATAIFA

Huduma za afya zinazotolewa chini ya usimamizi wa serikali za kigeni (za kitaifa na kiwilaya) na mashirika ya umma hazitahusika katika kuzingatia *sera hii*. Iwapo mipango ya sekta za serikali itasaidia shughuli za utoaji mimba “kama mbinu ya kupanga uzazi” au kushiriki katika shughuli zingine zisizo halali zinazohusiana na utoaji mimba, serikali na mashirika ya kiserikali na ya umma yatalazimika kuwa na akaunti tofauti kwa fedha za msaada wa afya wa kimataifa zinazotolewa na serikali ya Marekani kuhakikisha kwamba hazitumiki katika shughuli hizi zilizopigwa marufuku. Vifaa vya kitabibu vilivyoonuliwa na fedha za serikali ya Marekani na vile vile vituo vinavyosaidiwa na ufadhili huo haviwezi kutumiwa kutoa huduma za utoaji mimba usio halali. Asasi za kigeni isiyo ya kiserikali ambayo inatoa msaada kwa sekta ya serikali inahusika katika kuzingatia *sera hii*.

Kutohusika (au msamaha) katika kuzingatia *sera hii* kwa serikali za kigeni pia kunahusu vyo vikuu vya kitabibu na hospitali zinazoendeshwa na serikali, ambazo hutoa huduma za utoaji mimba kama sehemu ya mafunzo ya kutoa huduma kamilifu za afya au katika kufanya utafiti unaohusiana na utoaji mimba.

Masharti ya sera hii pia hayatatumiwa kwa kamati za ushauri za afya zinazodhaminiwa na serikali, kushiriki katika utafiti; uenezaji wa taarifa kwa umma kuhusu swala hili, visababishi au madhara ya utoaji mimba usio salama; na kushiriki katika kutengeneza sera za kitaifa zinazohusiana na utoaji mimba.

Mashirika ya kimataifa au yale yanayohusisha serikali mbalimbali kama vile Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), na vile vile “mashirika mengine ya kimataifa ambayo mataifa yanayojitawala hushiriki (kama vile Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, pamoja na Ushirika wa Chanjo Duniani - Gavi,” hayahusiki katika kuzingatia sera hii.

UTOAJI MIMBA KUFUATIA HALI INAYOHATARISHA MAISHA, UBAKAJI AU KUJAMIIANA KWA MAHARIMU

Asasi za kigeni zisizo kiserikali zinazostahiki kupata msaada wa afya wa kimataifa kutoka kwa serikali ya Marekani iwapo wanafanya utoaji mimba katika hali ambayo “maisha ya mama yangukuwa hatarini iwapo angebeba mimba hiyo hadi wakati wa kujifungua” au “kufuatia kubakwa au kujamiiana kwa maharimu.” Kwa mujibu wa masharti ya sera hii, utoaji mimba unaofanyika kwa sababu au hali nyingine yoyote kutakuwa marufuku, na kwa uwazi “afya ya kimwili na kiakili ya mama na utoaji mimba kufuatia hali zisizo za kawaida za kijusi.”

Hata hivyo, iwapo asasi ya kigeni isiyo ya kiserikali inayopokea ufadhili wa msaada wa afya wa kimataifa kutoka kwa serikali ya Marekani inapofanya utoaji mimba katika hali ambapo maisha ya mama yanahatarishwa, amebakwa au kujamiiana na maharimu, tendo hilo limeruhusiwa kwa uwazi chini ya sera hii, na asasi hiyo inapaswa kuandika taarifa kama kumbukumbu kuhusu hali na sababu iliyoitea kufanya shughuli hiyo ya kutoa mimba na jinsi asasi hiyo ilivyozingatia sheria ya nchi husika.

Kumiliki vifaa vya kupuliza hewa kwenye fuko la uzazi au kulipanua na kuondoa kijusi (D & C) au kumiliki dawa zinazofanya mama kutoa damu ya hedhi zinazotumiwa katika hali zinazohatarisha maisha ya mama, kubakwa au kujamiiana kwa maharimu au kutibu matatizo yatokanayo na mimba au baada ya kutoa mimba hakuwezi kusababisha asasi hiyo kutopata msaada wa afya unaotolewa na serikali ya Marekani. Hata hivyo, hairuhusiwi kutumia fedha za msaada kutoka serikali ya Marekani kununua au kusambaza vifaa hivyo.

USHAURI NA KUTOA RUFAA YA UTOAJI MIMBA

Rufaa na ushauri nasaha kuhusu utoaji mimba unaruhusiwa katika hali ambapo maisha ya mwanamke yako hatarini, kubakwa au kujamiiana na maharimu.

Katika nchi ambazo utoaji mimba ni halali kwasababu kubwa zaidi ya hali ya hatarishi kwa maisha ya mwanamke, kubakwa au kujamiiana na maharimu, mawasiliano ya wazi baina ya wanawake na watoaji wa huduma za afya yanakatazwa chini ya sera hii. Rufaa ya utoaji mimba katika hali zingine kama hizo inakubalika katika nchi hizo iwapo tu masharti yote manne yafuatayo yanatimizwa:

- Mwanamke tayari ana mimba;
- Mwanamke “anasema wazi kuwa tayari ameamua” kutoa mimba;
- Mwanamke “anauliza hususan” pale ambapo anaweza kupata huduma salama na halali ya utoaji mimba salama; na
- Mtoaji wa huduma ya afya ana sababu ya kuamini kuwa kanuni za maadili ya kimatibabu ya nchi zinamhitaji kutoa rufaa ya huduma salama na halali ya kutoa mimba.

Sharti moja la ziada lisilohusishwa katika vizuizi vya utoaji ushauri na rufaa ya utoaji mimba limejumuishwa kwenye sera hii. Asasi ya kigeni isiyo ya kiserikali haihatarishi ustahiki wake wa kupokea msaada wa afya wa kimataifa unaotolewa na serikali ya Marekani iwapo kuna hitaji la “kisheria la jukumu la mtoa huduma za afya” la kutoa ushauri na rufaa ya utoaji mimba chini ya sheria ya nchi husika kwa sababu zilizo kando na kuhatarisha maisha, kubakwa au kujamiiana na maharimu. Matumizi mapana na umuhimu wa kutohusika chini ya sera yanaelekea kuwa yenye maswali na yanayotegemea masharti yaliyopo sasa katika sheria za kitaifa. Hata hivyo, asasi za kigeni zisizo za kiserikali zinahimizwa kushauriana na watumishi wa serikali ya Marekani na mashirika yao katika nchi husika kuamua iwapo kutohusika na kuzingatia sera hii kuna tafsiri gani katika mazingira yao ya kitaifa au eneo husika.

UCHOCHEZI JUU YA UTOAJI MIMBA

Asasi za kigeni zisizo za kiserikali zinazopokea msaada wa afya wa kimataifa unaotolewa na Marekani haziwezi kushawishi serikali yao kuhatalisha au “kuendeleza uhalali” wa utoaji mimba kufuatia sababu zingine kando na kuokoa maisha ya mwanamke, kubakwa au kujamiiana na maharimu.

Aidha, asasi za kigeni zisizo za kiserikali zinazopokea Msaada wa Afya wa Kimataifa unaotolewa na Marekani haziwezi kufanya “kampeni ya kuhamasisha umma. . kuhusu faida na/au upatikanaji wa huduma ya utoaji mimba” ila katika hali za kuhatarisha maisha, kubakwa au kujamiiana na maharimu. Hata hivyo, sera hii haizuii matumizi ya utafiti wa kidemografia na afya kuhusu utoaji mimba ulioelezewa hapa chini na asasi fulani zisizo za kiserikali (kama vile shirika la Marekani lisilo la kiserikali au shirika la kigeni lisilo la kiserikali ambalo halipokei msaada kutoka serikali ya Marekani) ili kuchochea serikali za kigeni kuhatalisha utoaji mimba.

MAFUNZO NA VIFAA VYA KUTIBU MATATIZO YATOKANAYO NA UTOAJI MIMBA

Sera ya serikali ya Marekani inaruhusu waziwazi asasi za kigeni zisizo za kiserikali kutoa “matibabu ya majeraha au magonjwa yanayosababishwa na utoaji mimba kisheria au kinyume cha sheria kwa mfano utunzaji wa baada ya kutoa mimba.” Mashirika yanahimizwa kutoa matibabu ya matatizo yanayotokea baada ya kutoa mimba (k.m. maambukizi ya fuko la uzazi au utoaji mimba usiokamilika) wao wenyewe au kusaidia wateja kupata matibabu (k.m. kusindikiza mwanamke kwenda kwa hospitali).

Msaada wa USAID unaweza kutumia kusaidia katika mafunzo ya wahudumu wa afya kuwawezesha kutoa utunzaji wa baada ya uavyaji mimba, matibabu yenyewe na usaidizi mwingine wa kiufundi unaohusika. Lakini kulingana na sera ya shirika, fedha za USAID haziwezi kutumiwa kununua vifaa vya kutolea mimba (MVA) au matibabu mengine ili kutoa huduma za utunzaji wa baada ya kutoa mimba. Hata hivyo, hakuna masharti kwa mashirika asasi zisizo za kiserikali kutumia fedha zinazotokana na vyanzo vingine mbali na serikali ya Marekani ili kutimiza mahitaji ya USAID ya kuchangia gharama ili kununua vifaa vya MVA au bidhaa zingine za kutumiwa katika kutoa utunzaji wa baada ya kutoa mimba.

SERA YA SERIKALI YA MAREKANI INARUHUSU WAZIWAZI MASHIRIKA YA KIGENI YASIYO YA KISERIKALI KUTOA “MATIBABU YA MAJERAHA AU MAGONJWA YANAYOSABABISHWA NA UAVYAJI MIMBA HALALI NA USIO HALALI, KWA MFANO UTUNZAJI WA BAADA YA UAVYAJI MIMBA.”

USHAURI NA HUDUMA ZA KUPANGA UZAZI BAADA YA KUTOA MIMBA

Asasi zisizo za kiserikali zinaweza kupokea na kutumia msaada unaotolewa na serikali ya Marekani ili kutoa ushauri na huduma za uzazi wa mpango kwa wanawake ambao wamepoteza mimba bila kukusudia au waliotoa mimba kwa makusudi, ikiwemo kutoa mimba kinyume na sheria. Mashirika yanaweza kuwasiliana na kuratibu shughuli na asasi ya kigeni isiyo ya kiserikali, wakiwemo watoa huduma za utoaji mimba, ili kuwezesha kutoa huduma za uzazi wa mpango au za afya ya uzazi baada ya kutoa mimba.

UTAFITI WA KITABIBU WA KUTOA MIMBA

Kwa mujibu wa marufuku ya kisheria iliyopitishwa na Bunge la Marekani mnamo mwaka wa 1981, asasi zisizo za kiserikali—za Kimarekani na za kigeni—haziwezi kutumia fedha zinazotolewa na Marekani kufadhili utafiti wa kitabibu juu ya utoaji mimba. Asasi zisizo za kiserikali za Marekani, hata hivyo, zinaweza kutumia fedha zinazotokana na vyanzo vingine kufanya utafiti kama huo.

Utafiti wa aina yoyote haujatajwa kwa dhahiri katika masharti yanayotekeleza *sera hii*. Hata hivyo, ufasili wa “kuendeleza utoaji mimba kwa vitendo” katika masharti ni mfano tu, na sio orodha kamili ya shughuli (“inajumuisha, lakini sio tu, shughuli zilizo hapa juu”). Kuna ishara kwamba serikali ya Marekani inachukulia utafiti wa kitabibu wa utoaji mimba unaofanywa na asasi ya kigeni isiyo ya kiserikali, bila kujali chanzo cha ufadhili wake, kulifanya shirika hilo kutostahiki kupokea msaada wa afya wa kimataifa unaotolewa na serikali ya Marekani.

UTAFITI WA DEMOGRAFIA NA AFYA JUU YA UTOAJI MIMBA

Asasi za kigeni zisizo za kiserikali hazihatarishi ustahiki wao wa kupokea msaada wa afya wa kimataifa iwapo zinashiriki katika aina fulani za utafiti wa suala la utoaji mimba. Mbali na kuweka rekodi za taarifa za historia ya utoaji mimba za wateja, mashirika yanaweza kukusanya taarifa kuhusu matukio jumla ya utoaji mimba na visababishi vyake, madhara ya kiafya ya utoaji mimba kinyume na sheria vikiwemo vifo na majeraha, na gharama yake kwa mfumo wa utoaji wa huduma za afya. Aina hizi za utafiti wa magonjwa au za kutoa taarifa za kitafiti kuhusu dhana au ugonjwa fulani zinaweza kufadhiliwa na serikali ya Marekani.

Asasi za kigeni zisizo za kiserikali zinazopokea ufadhili wa afya wa kimataifa haziwezi kutumia matokeo ya utafiti huo (hata kama utafiti huo unafadhiliwa na serikali ya Marekani au la), au utafiti mwingine wowote, kufanya uchochezi au kampeni za kuhamasisha umma kuhusu kuhalalishwa kwa utoaji mimba au kuendeleza sheria za utoaji mimba kwa sababu zingine kando na kuhatarisha maisha ya mwanamke, kubakwa, au kujamiiana na maharimu. Lakini kustahiki kwa shirika hilo kwa kupokea msaada wa afya wa kimataifa unaotolewa na serikali ya Marekani hakuhatarishiwa kwa kushiriki tu kwa utafiti ambao unaweza kutumiwa na wengine kuendeleza marekebisho ya sheria ya utoaji mimba. Aidha, uenezaji wa matokeo ya utafiti wa kidemografia na wa afya unaohusu utoaji mimba kwa umma na asasi ya kigeni isiyo ya kiserikali unakubalika kwa sharti kuwa matokeo ya utafiti huo hayatatumiwa na asasi za kigeni zisizo za kiserikali kuunga mkono au kupendekeza kuondolewa kwa vizuizi katika sheria za utoaji mimba (k.m., katika makala ya jarida au machapisho mengine ambayo yanaweza kutolewa na kusambazwa na asasi hiyo ya kigeni isiyo ya kiserikali).

MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI YANAWENZA KUPOKEA NA KUTUMIA USAIDIZI UNAOTOLEWA NA SERIKALI YA MAREKANI ILI KUTOA USHAURI NA HUDUMA ZA UPANGAJI UZAZI KWA WANAWAKE AMBAO WAMEPOTEZA MIMBA BILA KUKUSUDIA AU WALIOAVYA MIMBA KIMAKUSUDI, IKIWEMO UAVYAJI MIMBA USIO HALALI.

UTAFITI WA MIPANGO YA AFYA NA KUIMARISHA MAAMUZI YA KIUTENDAJI

Ingawa haijatajwa au kuwekwa wazi katika sharti linalojumuishwa kwenye mikataba ya serikali ya Marekani ya ufadhili wa afya katika kutekeleza *sera hii*, asasi ya kigeni isiyo ya kiserikali inayoshiriki katika “utafiti wa kisayansi wa utekelezaji, utafiti wa mipango na operesheni, uchunguzi, tathmini za mahitaji na uimarishaji wa uwezo unaohusika unaofanywa kwa madhumuni ya kuboresha programu za msaada wa afya wa kimataifa unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani” ni lazima likubali sharti lililo katika mikataba yao ili kupokea msaada wa afya kutoka kwa Serikali ya Marekani, kulingana na mwongozo wa Wizara ya Mambo ya Nje uliotolewa kwa vyombo vya habari.

UTOAJI WA HUDUMA ZA UZAZI WA MPANGO

Sera hii haipigi marufuku asasi za kigeni zisizo za kiserikali kutoa mbinu yoyote inayopatikana ya uzazi wa mpango iliyoidhinishwa na Shirika la Kusimamia Vyakula na Madawa la Marekani (FDA), ikiwemo mbinu ya dharura ya uzazi wa mpango (EC), kama sehemu ya huduma za afya wanazotoa. Asasi zote zisizo za kiserikali zinazopokea msaada wa afya wa kimataifa zinaweza kutoa ushauri wa uzazi wa mpango, kutoa bidhaa na huduma za upangaji uzazi, na kuendeleza uhamasishaji wa mbinu za kupanga uzazi kulingana na sheria na sera za nchi husika.

MSAADA WA KIUFUNDI

Kwa mujibu wa *sera hii*, sharti la msaada wa kifundi linachukuliwa kama kuwekeza rasimali sawa na kutoa msaada wa kifedha kwa shirika jingine. Uhusiano wa utoaji msaada wa kiufundi katika mashirika unaashiria uhusiano endelevu na wenye umuhimu fulani unaohamisha kutoa stadi na kuimarisha uwezo wa asasi inayopokea msaada huo. Hata hivyo, ushirikiano wa hapa na pale baina ya mashirika (k.m. ziara, mashauriano, ukusanyaji wa data au mahojiano) haupaswi kuwekwa vizuizi kwa mujibu wa tafsiri ya *sera hii*.

VITENDO VYA MTU BINAFSI IKILINGANISHWA NA SHIRIKA

Masharti haya yanatumika kwa mashirika au asasi, sio kwa watu binafsi. Mtu binafsi aliye katika asasi au shirika lililo la kiserikali lakini linalolazimika kufuata *sera hii* anaweza kushiriki katika shughuli ambazo zinakubalika kama mtu binafsi lakini ingekuwa ni marufuku iwapo shughuli hizo zingetekelezwa na shirika lenyewe. Mtu binafsi anaweza kushiriki katika shughuli kama hizo ambazo zimewekewa marufuku ili mradi yeye “hayuko kazini au hafanyi shughuli hiyo kwenye majengo ya shirika,” shirika haliungi mkono au kufadhili kitendo hicho, na “hatua mahsusi” zinachukuliwa ili kuhakikisha mtu kama huyo “hawakilishi shirika kimakosa” kama kwamba anafanya hivyo kwa niaba ya shirika husika. [Pitia pia sharti lililoondolewa la mafunzo ya watu wanaohusika na asasi isiyo ya kiserikali lililoelezewa hapa juu.]

UZINGATIAJI WA MAJUKUMU YA UZINGATIAJI NA UFUATILIAJI

Mashirika yasiyo ya kiserikali ya Marekani yana wajibu wa kuhamishia masharti ya *sera hii* kwa mashirika ya kigeni yasiyo ya kiserikali wanaoshirikiana nao na ambayo yanapokea msaada wa afya wa kimataifa unaotolewa na Marekani kutoka kwao, na wa kufuatilia uzingatiaji wa washirika wao wa *sera hii*. Asasi za kigeni zisizo za kiserikali zina wajibu wa kuhakikisha uzingatiaji wao wenyewe wanapokea Msaada wa Afya wa Kimataifa moja kwa moja kutoka kwa Serikali ya Marekani, wa kuhamishia masharti ya *sera hii* kwa mashirika mengine yasiyo ya kiserikali wanayoshirikiana nayo ambayo hupokea msaada wa afya wa kimataifa unaogharimiwa na serikali ya Marekani, kama washirika wakuu, pamoja na kufuatilia uzingatiaji wa *sera hii* miongoni mwa washirika hao.

Hatua za kuhakikisha uzingatiaji zinaweza kujumuisha:

- Utengenezaji wa taratibu za kuchunguza asasi za kigeni zisizo za kiserikali katika hatua ya awali ya kuandika mchakato wa mradi;
- Uthibitisho wa ustahiki wa asasi ya kigeni isiyo ya kiserikali kupata msaada wa afya wa kimataifa unaotolewa na serikali ya Marekani na makubaliano ya kuzingatia katika *sera hiyo* katika mkataba wa kutoa msaada uliotiwa sahihi;
- Kurejea taratibu za kuzingatiwa ili kuhakikisha kwamba asasi za kigeni zisizo za kiserikali zinazingatia *sera hiyo*;
- Uzingatiaji wa mara kwa mara baada ya mradi kuanza kutekelezwa, pamoja na shughuli kama vile ziara za wafanyakazi walioko katika nchi, kanda au makao makuu husika na matumizi ya orodha ya vitu vya kuzingatiwa, na/ au kuripoti uzingatiaji katika ripoti za maendeleo ya mradi;
- Kutoa elimu na mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu *sera* ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo ya mafunzo na nyenzo zingine za kutoa taarifa; na
- Kuunda taratibu za shirika za kutambua ukiukwaji na kuchukua hatua ya marekebisho.

MAELEZO ZAIDI

Vyanzo vya maelezo yaliyomo kwenye kipeperushi hiki ni pamoja na hati zifutazo:

- “Sera ya jiji la Mexico— Agizo la Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri wa Afya na Huduma za Kibinadamu, na Kiongozi wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani,” 23 Januari 2017.
<https://www.whitehouse.gov/the-press-office/2017/01/23/presidential-memorandum-regarding-mexico-city-policy>
- Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nchi (<https://www.state.gov/r/pa/prs/ps/2017/05/270866.htm>) na nukuu ya maelezo mafupi ya usuli yaliyotolewa na wasimamizi wa ngazi ya juu (<https://www.state.gov/r/pa/prs/ps/2017/05/270879.htm>), mnamo tarehe 15 Mei 2017.
- Wizara ya Nje, Shirika la Idadi ya Watu, Wakimbizi, na Uhamaji, “Utekelezaji wa Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya wa Kimataifa (Awali Ikijulikana kama ‘Sera ya jiji wa Mexico’),” Mwongozo Unaotolewa kwa Vyombo vya Habari wa PRM, 15 Mei 2017.
https://pai.org/wp-content/uploads/2017/09/FINAL-MCP-Press-Guidance_2017-05-14.pdf

Ujumbe wa ndani ya nchi kuhusu utekelezaji wa *sera*, ikiwa ni pamoja na:

- Wizara ya Mambo ya Nje, Shirika la Usimamizi, Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Ununuzi, “Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya wa Kimataifa,” Nambari 2017-01 ya Taarifa ya Ushauri ya Usimamizi wa Msaada wa Serikali Kuu, tarehe 15 Mei 2017.
https://pai.org/wp-content/uploads/2017/09/FAMA-2017_01-Protecting-Life-in-Global-Health-Assistance.pdf
- Katibu Mtendaji wa USAID, “Utekelezaji wa Sera ya kulinda Maisha katika Msaada wa Afya wa Kimataifa (awali ikiitwa Sera ya Mji wa Mexico),” USAID/Notisi ya Jumla, tarehe 15 Mei 2017.
https://pai.org/wp-content/uploads/2017/09/Implementation-of-Protecting-Life-in-Global-Health-Assistance_USAIDGeneral-Notice.pdf
- Vipengele vya masharti vilivyojumuishwa katika mikataba ya USAID na mashirika yasiyo ya kiserikali, ikiwemo marekebisha ya utekelezaji wa *sera*. Pitia Marekani, USAID, “Kulinda Maisha katika Usaidizi wa Afya wa Kimataifa (Mei 2017)” sehemu (kurasa 83-93) inayopatikana katika “Masharti ya Wastani ya Lazima kwa Wapokeaji wa Ufadhili wasio mashirika au asasi zisizo za kiserikali za Marekani.”
<https://www.usaid.gov/sites/default/files/documents/1868/303mab.pdf>
- Ili kupata taarifa kamili ya masharti yatakayojumuishwa katika mikataba ya msaada wa afya wa kimataifa baina ya mashirika yasiyo ya kiserikali na idara na taasisi nyingine husika za Marekani, tafadhali pitia:
 - Wizara ya Mambo ya Nje <https://www.state.gov/documents/organization/271867.pdf>
 - NIH: <https://grants.nih.gov/policy/protecting-life-global-health-assistance.htm>
 - CDC: <https://www.cdc.gov/grants/additionalrequirements/ar-35.html>
- Ili kupata taarifa kuhusu vikwazo vya kisera na kisheria juu ya msaada wa serikali ya Marekani kwa mashirika au asasi za nje, pitia tovuti ya USAID inayoelekeza maswala ya utoaji mimba vizuizi vya kisera
<https://www.usaid.gov/what-we-do/global-health/cross-cutting-areas/legislative-policy-requirements>
- Kuhusu kulinda uhiari katika kuamua juu ya chaguo lako baada ya kupata taarifa, pitia tovuti ya USAID ifuatayo
<https://www.usaid.gov/what-we-do/global-health/family-planning/voluntarism-and-informed-choice>
- Ili kupata mengi kuhusu mafunzo kwa njia ya kieletroniki Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya wa Kimataifa, tembelea tovuti ifuatayo <https://www.globalhealthlearning.org/course/protecting-life-global-health-assistance-and-statutory>

Kwa matumizi rasmi ya masharti ya serikali ya Marekani yanayoathiri msaada wa afya wa kimataifa, mashirika yanapaswa kushauriana moja kwa moja na idara au shirika la serikali ya Marekani linalotoa msaada husika. Hii ni pamoja na anuani za mawasiliano za watumishi katika makao makuu yaliyoko Washington na walioko katika ofisi za serikali katika nchi mbali mbali.

Ili kupata nakala za hati zilionukuliwa au kurejelewa katika mukhtasari huu, ili kupata msaada wa kuelewa sera za sasa za Serikali ya Marekani, au kuwasilisha taarifa kuhusu mambo ambayo mashirika hukumbana nayo katika utekelezaji wa *sera hii*, tafadhali wasiliana na PAI kupitia barua pepe ya PLGHA@pai.org au kwa njia ya simu kwa (202) 557-3400.

ILANI YA KUJIONDOLEA MAKOSA

Hakuna taarifa yoyote iliyomo kwenye kipeperushi hiki inapaswa kufasiriwa kwa njia dhahiri au sio dhahiri, kuwa uungaji mkono wa sera hii kwa upande wa PAI, Bodi yake ya Wakurugenzi, au wafanyakazi wake *sera hii* au utekelezaji wake na kuhakikisha inatekelezwa na serikali ya Marekani.

Yaliyomo kwenye kipeperushi yana nia ya kutoa maelezo ya jumla tu na hayapaswi kuzingatiwa kama ushauri wa kisheria. Ushauri wa kisheria unapatikana bila malipo. Tafadhali wasiliana na PAI ili uelekezwe kwa mawakili ambao wako tayari kutoa ushauri kwa asasi zisizo za kiserikali kuhusu *sera hii*.

Aidha, mashirika yasiyo ya kiserikali yanapaswa kushauriana na wafadhili wao nje ya Serikali ya Marekani pamoja na mikataba ya ufadhili ili kuamua uwezekano wa matumizi ya *sera hii* katika shughuli zao zisizofadhiliwa na serikali ya Marekani.

JE, MASHARTI YA SERA YANATUMIKA?

NDIYO	HAPANA
MIPANGO YA MISAADA*	
<ul style="list-style-type: none"> VVU/UKIMWI, ikiwemo Mpango wa Msaada wa Dharura wa Rais wa Kupambana na UKIMWI (PEPFAR) Kifua kikuu Malaria, ikiwemo Mpango wa Kupambana na Malaria Ulionzishwa na Rais (PMI) Janga la homa ya mafua na hatari zingine, ikiwemo kulinda afya ulimwenguni Hatari nyingine za afya ya umma, ni pamoja na magonjwa yaliyopuuzwa ya nchi za tropiki na mengine ya kuambukiza; magonjwa yasiyoambukizwa na uimarishaji wa mfumo wa afya Afya ya mama na mtoto, pamoja na maji, usafi wa mazingira na mwili, na maji (WASH) katika ngazi ya kaya. Uzazi wa mpango na afya ya uzazi Lishe 	<ul style="list-style-type: none"> Msaada wa kibinadamu, ikiwemo Msaada wa Serikali ya maswala ya uhamaji na wakimbizi na USAID pamoja na Idara ya Ulinzi ya maafa na misaada ya kibinadamu. Msaada wa Maendeleo Miundo mbinu ya maji na usafi na huduma zinazofadhiliwa na msaada wa maendeleo Msaada wa chakula (P.L. 480) Mpango wa Shule na Hospitali za Marekani zilizoko Nje ya Nchi
AKAUNTI ZA BAJETI AU ZA MATUMIZI YA FEDHA ZA SERIKALI	
<ul style="list-style-type: none"> Programu ya Afya ya Kimataifa (GHP) Mpango wa Msaada wa Dharura wa Rais wa Kupambana na UKIMWI (PEPFAR) Fedha za Msaada wa Kiuchumi (ESF) Msaada kwa nchi za Ulaya ya Mashariki, Urasia na Asia ya Kati (AEECA) 	<ul style="list-style-type: none"> Msaada wa Maendeleo (DA) Mpango wa Msaada kwa Uhamiaji na Ukimbizi (MRA) Mpango wa Msaada wa Majanga wa Kimataifa (IDA) Chakula kwa ajili ya Amani Msaada namba II (P.L. 480) Mfuko wa Fedha za Dharura za Misaada ya Uhamaji na Wakimbizi aa Marekani (ERMA)
MASHIRIKA NA MAKUNDI	
<ul style="list-style-type: none"> Asasi zisizo za kiserikali za nje, zote – za kibiashara na zisizo za kibiashara. 	<ul style="list-style-type: none"> Serikali za kigeni Mashirika yanayoshirikisha nchi mbalimbali Asasi zisizo za kiserikali za Marekani Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria, pamoja na Ushirika wa chanjo wa GAVI
MBINU ZA KUTOA MSAADA KWA ASASI ZISIZO ZA KISERIKALI ZA NCHI ZA KIGENI	
<ul style="list-style-type: none"> Misaada Mikataba ya Ushirikiano Mikataba ya Misaada Mikataba (ambayo haikutekelezwa kufikia tarehe 30/9/17) 	<ul style="list-style-type: none"> Misaada midogo kutoka kwa serikali ya kigeni Hati za ununuzi za bidhaa na huduma halisi zisizo na uhusiano wa moja kwa moja na utoaji wa Msaada wa Afya wa Kimataifa (k.m., usafirishaji wa meli)
AINA ZA MISAADA NA USAIDIZI	
<ul style="list-style-type: none"> Ufadhili Msaada wa kiufundi Bidhaa Mafunzo ya muda ya kujiendeleza kitaaluma Vifaa Mafunzo (hususan—iwapo yanaimarisha uwezo wa shirika) 	<ul style="list-style-type: none"> Mikopo Ushirikiano wa muda mfupi (k.m., mashauriano, mahojiano, ukusanyaji wa taarifa, chapisho) Bidhaa au huduma zilizounuliwa (k.m. kompyuta, usimamizi, bidhaa za ofisini)
WATU BINAFSI WANAPOKEA MSAADA	
<ul style="list-style-type: none"> Mhusika wa asasi isiyo ya kiserikali akiwakilisha asasi isiyo ya kiserikali Wahusika wa asasi isyo ya kiserikali wakishiriki katika mafunzo maalum 	<ul style="list-style-type: none"> Wahusika wa asasi isiyo ya kiserikali wakiwa katika hali ya watu binafsi Wahusika wa asasi isiyo ya kiserikali wanaoshiriki katika “programu ya mafunzo ya jumla”

* Pitia Wizara ya Nchi za Nje ya Marekani, Shirika la Usimamizi, Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Ununuzi, “Kulinda Maisha katika Msaada wa Afya wa Kimataifa,” Nambari 2017-01 ya Taarifa ya Ushauri ya Usimamizi wa Msaada wa Serikali Kuu, tarehe 15 Mei, 2017 na kitengo cha afya katika Muundo wa Programu ya Misaada kwa Mashirika na Asasi za Kigeni (<https://www.state.gov/f/releases/other/255986.htm#HL>)

SHUGHULI ZINAZOKUBALIKA ZINAZOHUSIANA NA UTOAJI MIMBA KWA MUJIBU WA SERA HII AU SHERIA ILIYOKO SASA

UFUNGUO

✓ Shughuli inayokubalika kwa mujibu wa marekebisha ya Sheria ya Helms ya mwaka wa 1973, *sera hii*, au marufuku ya sera nyingine zinazotumika.

☆ Shughuli inayokubalika chini ya sheria na sera ya sasa, lakini si dhahiri iwapo au ni mara ngapi (ikiwa itawahi tokea) asasi isiyo ya kiserikali ya Marekani litatoa huduma moja kwa moja kwa wateja bila kutegemea asasi ya kigeni isiyo ya kiserikali kama mshirika mkuu au wa kati.

* Shughuli zinazokubalika tu chini ya vipengele maalum sana (pitia maelezo kwenye kipeperushi hiki ili kupata maelezo ya kina zaidi kuhusu “rufaa zisizo amilifu”.

✚ Utafiti wa aina yoyote haujatajwa kwa dhahiri katika vipengele vinavyotekeleza *sera hii*. Hata hivyo, ufasili wa “kuchochea utoaji mimba” katika vipengele vya sera ni mifano tu, na sio orodha kamilifu ya shughuli (“inajumuisha, lakini sio tu, kwa shughuli zilizo hapa”). Inaonekana kwamba serikali ya Marekani inachukulia utafiti wa kitabibu unaohusu utoaji mimba unaofanywa na asasi ya kigeni isiyo ya kiserikali, bila kujali chanzo cha ufadhili wake, ni kigezo tosha cha asasi hiyo kutostahiki kupokea msaada wa afya unaotolewa na serikali ya Marekani. Aidha, pitia pia ujumbe katika kipeperushi hiki ili kupata maelezo kuhusu matumizi ya *sera hii* katika mbinu za kisayansi za utekelezaji na utafiti wa kuboresha maamuzi ya kiutendaji.

Asasi za kigeni zisizo za kiserikali zinapaswa kushauriana na wafadhili wao wengine ambao sio Serikali ya Marekani, na mikataba yao ya ufadhili ili kuamua ni shughuli zipi zinazokubalika.

AINA YA SHUGHULI

Kutoa Mimba

- Fanya utoaji mimba katika hali inayohatarisha maisha ya mwanamke, kufuatia ubakaji au kujamiiana na maharimu
- Fanya utoaji mimba iwapo mwanamke ana matatizo mengine ya kiafya (afya ya kimwili na ya kiakili), “matatizo ya kijusi”, na sababu za kijamii na kiuchumi au unapoombwa kufanya hivyo

Utoaji ushauri nasaha na Rufaa

- Toa rufaa ya kutoa mimba, iwapo ni halali
- Toa ushauri nasaha kuhusu utoaji mimba
- Ushauri nasaha, rufaa na huduma za kupanga uzazi za baada ya kutoa mimba

Kushawishi

- Kushawishi serikali ya kigeni kuhalalisha au “kuendeleza uhalali” wa utoaji mimba kwa sababu zingine mbali na kuhatarisha maisha ya mwanamke, kubakwa au kujamiiana na maharimu
- Fanya kampeni za “kutoa taarifa kwa umma . . . kuhusu faida na/au upatikanaji wa huduma za utoaji mimba” kwa sababu mbali na zile zinazohatarisha maisha ya mwanamke, kubakwa au kujamiiana na maharimu

Huduma ya afya ya kutoa mimba

- Ununuzi wa vifaa vya kutolea mimba (MVA)
- Kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya kuhusu matibabu ya matatizo yanayoweza kutokea baada ya kutoa mimba (k.m. maambukizi ya fuko la uzazi kutokana na utoaji mimba usiokamilika)
- Toa msaada wa kuimarisha mifumo ya usambazaji wa vifaa inayojumuisha vifaa vya kutoa mimba (MVA) vya kutumiwa katika kipindi cha baada ya kutoa mimba

Utafiti ✚

- Fanya utafiti wa kitabibu kuhusu utoaji mimba
- Shiriki katika utafiti wa kidemografia, hali ya magonjwa katika jamii au sayansi ya jamii kuhusu mada ya utoaji mimba

ASASI YA KIGENI ISIYO YA KISERIKALI		ASASI ISIYO YA KISERIKALI YA KIMAREKANI	
MSAADA UNAOTOLEWA NA SERIKALI YA MAREKANI	MSAADA USIOTOLEWA NA SERIKALI YA MAREKANI	MSAADA UNAOTOLEWA NA SERIKALI YA MAREKANI	MSAADA USIOTOLEWA NA SERIKALI YA MAREKANI
✓	✓	☆	☆ ☆
* ✓	* ✓	✓ ✓ ✓	✓ ✓ ✓
			✓ ✓
✓ ✓	✓ ✓	✓ ✓	✓ ✓ ✓
✓	+ ✓	✓	✓ ✓


KUHUSU PAI

PAI hutetea sera ambazo huwezesha wanawake kutumia haki zao za uzazi, na kupambana na kuondoa vikwazo vya kiseru ili wanawake waweze kupata huduma za kiafya wanazohitaji. Tunashirikiana na watunga sera jijini Washington na mtandao wetu wa washirika walio katika nchi zinazoendelea ili kuendeleza haki za uzazi za wanawake. Shirika la PAI, lililoanzishwa mwaka wa 1995, ni kundi lisilo la kibiashara na halipokei ufadhili wowote kutoka kwa serikali ya Marekani.

Kwa taarifa zaidi kuhusu sera hii, tembelea tovuti www.pai.org

**CHAMPIONS
OF GLOBAL
REPRODUCTIVE RIGHTS**
pai.org

1300 19th Street NW, Suite 200
Washington, DC 20036-1624 USA
(202) 557 3400
www.pai.org • info@pai.org

 @paiwdc
 @pai_org
 @pai_insta